# OFISI YA RAISI TAMISEMI.

## HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE

## SHULE YA SEKONDARI **ULEMBWE.**

S.L.P 582,

**NJOMBE.**

06/12/2020

**0754630967.**

**NDUGU……………………………………………**

S .L .P ……………………….

**YAH:-MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI ULEMBWE.**

**UTANGULIZI**.

Ninayofuraha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Ulembwe ipo umbali wa kilometa 12 kusini magharibi mwa mji mkuu wa mkoa wa Njombe, halmashauri ya wilaya ya Wanging'ombe, kata ya Ulembwe.

Muhula wa masomo utaanza tarehe **11/01/2021**. Utatakiwa kifika shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti itakuwa tarehe **25/01/2021** (ndani ya wiki mbili).

**MAMBO MHIMU YA KUZINGATIA.**

**A: SARE ZA SHULE.**

**WAVULANA.**

i) Mashati mawili (2) meupe ya mikono mirefu.

ii) Suruali mbili(2) moja rangi ya damu ya mzee na nyingine dark blue – mshono wa kawaida na zisiwe modal wala za kubana na kitambaa kiwe namba 1.

iii) Viatu vyeusi vya kamba visivyo na kisigino kirefu jozi 2.

iv) Soksi nyesi jozi mbili au zaidi.

v) Mkanda mweusi wa ngozi.

vi) Sweta moja rangi ya kijani ya jeshi, lenye shingo ya V.

vii) Sweta moja kaba shingo langi nyeusi.

viii) Nguo za ndani za kutosha na leso mbili.

**WASICHANA**

i. Blauzi 2 nyeupe za mikono mirefu.
ii. Suruali 2 (moja rangi ya damu ya mzee na nyingine rangi ya dark blue ) mshono wa kawaida isiyobana.
iii. Gauni mbili 2,moja ya damu ya mzee na nyingine light blue(bulue bahari) mshono wa gauni –shingo ya mduara(round) bila mikono na marinda 14 kuanzia kiunoni hadi chini ya magoti na sio juu ya magoti.
iv. viatu vya kamba vyeusi jozi mbili vyenye kisigino kifupi (sio yebo wala bajaji)
v. Soksi nyeupe jozi 2 za kawaida na sio fupi
vi. Sweta moja rangi ya kijani ya jeshi lenye shingo ya V
vii. Nguo za ndani(chupi). zaidi ya 4 na tighti angalau 2 au zaidi.
viii. Leso mbili au zaidi
ix. Sweta kabashingo PULL NECK nyeusi moja.

**ZINGATIO**: Rangi ya hijabu kwa wale waisilam ziwe nyeupe.

**NGUO ZA MICHEZO KWA WAVULANA NA WASICHANA.**

i) Track suti nyeusi

ii) Raba jozi moja.

**MAHITAJI YA HOSTEL KWA WASICHANA NA WAVULANA.**

I. Godoro futi 2.5 lenye foronya na mto wake.
II. Blanketi moja zito
III. Mashuka mawili,moja rangi ya pink,na lingine rangi ya blue bahari.
IV. Mchango wa kitanda ni TSH 10,000/-iingizwe bank kwenye akaunti ya shule iliyoandikwa sehemu ya mchango wa chakula katika barua hii.
V. Chombo cha chakula kontena lenye mfuniko na kijiko.
VI. Vifaa vya usafi binafsi(mswaki na dawa yake,Sabuni za kutosha,kiwi,kandambili, Taulo mafuta ya kujipaka, ya kawaida na sio marashi, Ndoo moja ya lita 10 na chanuo)
VII. Tochi moja yenye betri au inayotumia mwanga wa jua (kwa dharura)
VIII. Khanga doti moja kwa wasichana na Taulo za kike( pads) za kutosha.

**NGUO ZA KUSHINDIA AU ZA KAZI.**

a)Wavulana –Suruali moja rangi ya khaki
T-shirt mbili nyeupe
Jaketi jeusi kwa msimu wa baridi tu.

b)Wasichana.-Sketi moja ndefu rangi ya khaki
T-sirt mbili nyeupe
Jaketi jeusi kwa msimu wa baridi tu.

MICHANGO YA CHAKULA KWA WANAFUNZI WA HOSTEL.

1. Mahindi debe 10 kwa mwaka, nusu mwaka debe 5.
2. Maharage debe 2.5 kwa mwaka, nusu mwaka debe 1.5
3. Mchele debe 1 kwa mwaka, nusu mwaka kilo 10.
4. Fedha ya viungo 100,000/ nusu mwaka 50,000/-

UNARUHUSIWA KULIPA NUSU KWA KILA MCHANGO KWA MWAKA. FEDHA ZOTE ZILIPWE BENKI KWA NAMBA **60602300243 NMB**, JINA LA AKAUNTI ULEMBWE SEKONDARI. KISHA LETA KARATASI YA

BANKI (BPS)SHULENI ILI UPEWERISTI YA SHULE. KUMBUKA KUANDIKA JINA LA MWANAFUNZI UNAYEMLIPIA NA KIDATO CHAKE.

**VIFAA VYA MASOMO.**

i. Daftari kubwa counter books Q2 au zaidi 10 na ndogo 10 kwa ajili ya mazoezi.
ii. Mkebe wenye vifaa vyote kwa somo la hisabati.
iii. Kamsi ya kiingereza (Dictionary)
iv. Kalamu za wino blue au nyeusi, pensel na rula.
v. Bunda 1 la kalatasi RIM A4 kwa ajili ya mitihani na majaribio ya mwezi,wiki na muhula.

VIFAA VYA USAFI.

i. Jembe moja lenye mpini kwa wavulana wote.
ii. Mfagio 1, kwa ajili ya sakafu kwa wasichana wote.
iii. Mfagio wa chelewa 1 kwa wavulana na wasichana.

SHERIA NA KANUNI MHIMU ZA SHULE.

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25. ya mwaka 1978 na kama ilivyolekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu,sayansi na technologia yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

SHERIA ZA SHULE.

1. Fika shuleni kila siku saa 1:00 asubuhi kwa siku za masomo.
2. Fanya usafi wa maeneo uliopangiwa kabla kipindi kinachofuata kuanza.
3. Hudhuria vipindi vyote vya shule kwa kuzingatia ratiba iliyopangwa.
4. Kuwa msafi kwa mawazo,maneno,matendo, nguo na mwili muda wote.
5. Ukiwa na tatizo muone mwalimu yeyote uliye karibu nae ili akusaidie vizuri na haraka.
6. Uwapo shuleni huruhusiwi kubadili jina.
7. Huruhusiwi kubadili dini uwapo shuleni hadi idhini itolewe na mzazi wako.
8. Tabia ya kutoroka vipindi haitavumilika,ukibainika utachukuliwa hatua za kinidhamu.
9. Utatakiwa kuwa katika sare kamili uwapo shuleni muda wote.
10. Kutii kengele na kuwahi kufika mahali unapotakiwa.
11. Ugomvi,matusi,na unyanyasaji wa aina yoyote hauruhusiwi kabisa.
12. Huruhusiwi kuja na vazi la aina yoyote ambalo halihusiani na sare ya shule kama upo hosteli.
13. Simu ni marufuku kwa mwanafunzi shuleni, ukuonekana nayo utanyang’anywa na utaivunja mwenyewe mbele ya wanafunzi.
14. Shule itatoa namba ya simu ya shule kwa mawasiliano na ndugu au wazaziambapo tutarekodi namba zote unapopiga ili kuhakiki usahalali wa namba hizo.

KUFUKUZWA SHULE.

Makosa yanayoweza kusababisha kufukuzwa shule mara moja ukibainika nayo ni haya:-

1. Wizi
2. Uasherati, Ubakaji, na Ushoga.
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.

4. Uvutaji bangi.
5. Makosa ya jinai.
6. Kupigana au kupiga.
7. Kudharau bendera ya Taifa.
8. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
9. Kuoa au kuolewa.
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
11. Kutoa au kusaidia kutoa mimba.
12. Kugoma,kuchochea, au kuongoza kuvuruga amani na usalama wa watu.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.
14. Kutoroka shuleni.

NB : Tafali zingatia kuwa michango,chakula na vifaa vyote vilivyoagizwa vitakaguliwa siku ya kufungua shule/kuripoti.

HALMASHAURI YA WILAYA YA WANGING'OMBE.

SHULE YA SEKONDARI ULEMBWE,

S L P 582

NJOMBE.

MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI.

(JAZA KWA HERUFI KUBWA TU)

1.Jna la mwanafunzi (majina matatu)…………………………………………………….

Tarehe ya kuzaliwa ……………………mahali alipozaliwa kijiji ………………………

Wilaya ………………………..Mkoa ……………………………………………………

Dini yako ……………………………..Dhehebu…………………………………………

Shule uliyotoka……………………………………………………………………………

2. Jina la Baba …………………………………………..Yu hai / alifariki……………..

Jina la Mama …………………………………………Yu hai /alifariki………………

Jina la mlezi kama baba arifariki…………………………………………………………...

Anwani ya Baba mzazi /mama /Mlezi……………………………………………………..

Kazi afanyayo Baba mzazi/mama /Mlezi …………………………………………………

(futa lisilohusika)

Jina la mwajiri kama ameajiriwa………………………………………………………….

Dini ……………………………Dhehebu…………………………………………………

Namba ya simu ya Baba mzazi/Mama /Mlezi ……………………………………………

**FIKA NA FOMU HII SIKU YA KURIPOTI.**